Policy brief TZ.10/2010E

# Je, Tanzania ikope kibiashara?






## 1. Utangulizi

Katika kitabu chake ambacho kimeibua mijadala mingi, *"Dead Aid: Why aid is not working and how there is a better way for Africa"* Dambisa Moyo[1] ana pendekezo mahsusi kuhusu namna nchi za Kiafrika zinavyoweza kujikwamua kutoka katika lindi la matatizo yanayotokana na tasnia ya misaada ya kigeni: nchi kukopa kibiashara, na kusimamia maendeleo yao kikamilifu. Je, Serikali ya Tanzania inaweza kuwa imeupokea ujumbe huu?

Wakati wa kuwasilisha mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2010/11 Bungeni mwezi Juni 2010, Waziri wa Fedha alitangaza nia ya serikali ya kukopa, si tu kutoka vyanzo vilivyozoeleka bali pia kukopa kibiashara. Nia ya kukopa kibiashara iliwekwa bayana kwa mara ya kwanza katika mwaka wa fedha wa 2007/08 lakini haikuweza kutekelezeka kutokana na msukosuko ulioyakumba masoko ya fedha ya kimataifa katika kipindi hicho. Sasa wazo hilo limeibuliwa tena.

## 2. Deni la taifa: Tanzania iko katika nafasi gani?

Mwishoni mwa mwezi Juni 2010, jumla ya deni la Tanzania ilifika dola za Marekani bilioni 9.9. Kulingana na viwango vya kubadilisha fedha katika mwezi huo wa Juni, kiasi hicho kilikuwa sawa na shilingi trilioni 13.6 (Tazama Kielelezo cha 1). Ni sawa na kusema kuwa mpaka mwezi Juni 2010 kila Mtanzania alikuwa anadaiwa na wakopeshaji kiasi cha shilingi za Tanzania 332,000 kupitia deni hilo la taifa.

Katika mwaka wa fedha wa 2010/11 Serikali itakopa shilingi bilioni 2,128.832 (trilioni 2.1) kwa masharti ya kibiashara kutoka ndani na nje ya nchi. Katika kiasi hiki cha fedha, shilingi bilioni 797.62 sio deni jipya: Serikali itauza dhamana na hati fungati ili kulipia dhamana zinazoiva. Kimsingi Serikali inapofanya hivi hailipunguzi deni lake; badala yake inaliweka karibu katika kiwango kilekile. Fedha nyingine, shilingi trilioni 1.3 zitakuwa deni jipya ambalo kwa mujibu wa Waziri wa Fedha litagharimia miradi ya maendeleo ya miundombinu. Kukiwa na kiasi kingine cha shilingi trilioni 1.21 kinachokopwa kwa wafadhili kwa masharti nafuu, jumla ya deni inatarajiwa kukua kwa kiasi cha


Muhtasari huu umeandaliwa na Uwazi-Twaweza
Iliyopo Hivos Tanzania

Uwazi, S.L.P 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
Simu +255 22 266 4301. Nukushi +255 22 266 4308.
Barua pepe: info@uwazi.org. Tovuti: www.uwazi.org

Muhtasari ulitolewa kwa lugha ya Kiingereza Oktoba 2010
na kutafsiriwa kwa Kiswahili Aprili 2011

kama shilingi trilioni 2.54 au shilingi 54,000 hivi kwa kila Mtanzania, pungufu au zaidi kidogo ifikapo Juni 2011.

**Kielelezo cha 1: Jumla ya deni la taifa**





**Chanzo:** Ukokotoaji wa waandishi kwa kutumia taarifa kutoka majarida ya Takwimu ya Benki Kuu

# 3. Kukopa kibiashara, upo uwezekano tena

Uwezekano wa Tanzania kukopa kwa masharti ya kibiashara umefungua fursa mpya ambayo haikuwepo kwa kipindi kirefu kilichopita. Bila misamaha mikubwa ya madeni, ambayo kwa kiasi kikubwa ilitekelezwa kati ya 2000 na 2007 chini ya mpango wa kusaidia nchi masikini zenye madeni makubwa kuondokana na mzigo mkubwa wa madeni ya kigeni [(*the Highly Indebted Poor Countries (HIPC) initiative*) na *Multilateral Debt Relief Initiative (MDRI)]*, uwezekano wa Tanzania kukopa kwa masharti ya kibiashara ungebakia kuwa ndoto. Hii ni kwa sababu wakati huo Tanzania ilikuwa na mzigo mkubwa wa madeni na hivyo ilikuwa haikopesheki. Kuna wakati katika miaka ya mwisho ya 1990 ambapo uwiano wa deni la nje kwa pato la taifa ulipanda hadi kufikia zaidi ya asilimia 100; na uwiano wa deni la nje kwa mapato yatokanayo na uuzaji wa bidhaa nchi za nje ulikuwa zaidi ya asilimia 500 (Tazama Kielelezo cha 2). Wakopeshaji wa kibiashara wakasitisha kutoa mikopo kwa Tanzania. Matokeo yake ni kwamba mikopo yenye masharti nafuu na msaada kutoka kwa wafadhili na taasisi za kimataifa za fedha vikawa ndivyo nyanzo kikuu vya kulipia nakisi ya fedha iliyokuwepo katika matumizi ya Serikali.

**Kielelezo cha 2: Uwiano wa deni la Taifa kwa Pato la Taifa (GDP) na mapato ya biashara za nje**




**Chanzo:** Ukokotoaji wa waandishi kwa kutumia taarifa kutoka majarida ya Takwimu ya Benki Kuu

Kutokana na misamaha ya madeni viashiria vya uwezo wa Tanzania kuhimili ulipaji wa madeni vimeimarika. Kasi ya kukua kwa pato la taifa (GDP) na ukuaji wa biashara za nje kwa pamoja vimesaidia kuimarisha zaidi uwiano wa deni la taifa kwa pato la taifa, na deni la taifa kwa mapato yatokanayo na biashara za nje kiasi kwamba uchambuzi wa deni la Tanzania uliofanywa kwa ushirikiano wa Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) na Benki ya Dunia unaonesha kuwa uwezekano wa Tanzania kushindwa kabisa kuhimili madeni yake ni mdogo. Kutokana na hali hii, sasa Tanzania inaweza kukopeshwa kibiashara.[2]

# 4. Tanzania inaweza kukopa kibiashara, lakini je, ifanye hivyo?

Je, fursa ya kukopa kibiashara ikumbatiwe? Na je, Tanzania iko katika mazingira gani kuhusu uwezekano wa kutumbukia tena katika hali ya ukopaji/madeni isiyo endelevu?

Takwimu za hivi karibuni hazioneshi uwezekano wa Tanzania kutumbukia tena katika hali ya ukopaji madeni isiyo endelevu katika siku zijazo za karibuni: wiano zote mbili, deni-pato la taifa na deni-mapato ya biashara za nje ziko katika viwango vizuri. Hata hivyo, Serikali isisahau ukweli kwamba kila shilingi inayokopa ni dhima ambayo Watanzania watailipa kupitia kodi zaidi. Kwa ajili hiyo, viashiria vya uendelevu wa uwezo wa kulipa madeni lazima vidumishwe katika hali nzuri kwa kuimarisha ukuaji wa biashara za nje na pia ukuaji wa pato la taifa.

Vilevile, uwekezaji unaofanywa kwa kutumia fedha za mikopo unapaswa kuhakikisha kwamba thamani bora inapatikana kwa fedha zinazotumika, na kwamba uwekezaji huo unawanufaisha wananchi wake katika hali ya usawa. Iwapo uwekezaji unaofanyika utashindwa kutimiza kigezo hiki katika hatua ya upangaji na katika hatua yake ya utekelezaji, basi kutakuwa na uwezekano mkubwa kwa Tanzania kwa siku za karibuni kuingia tena katika hatari ya kulimbikiza deni lisilo endelevu.

Historia ina somo muhimu la kutufundisha kuhusiana na jambo hili. Sehemu kubwa ya deni lililolimbikizwa kabla ya kipindi cha msamaha wa deni ni mikopo ambayo haikutumiwa vizuri, na ni baadhi tu ya makundi katika jamii au maeneo ndiyo yalinufaika nayo. Upungufu mkubwa katika upatikanaji na ubora wa miundombinu unaoikabili Tanzania licha ya deni kubwa ambalo nchi ililimbikiza katika miaka hiyo, unathibitisha ukweli huu. Hata hivyo, ilikuwa ni lazima deni lilipwe, isipokuwa tu pale ambapo wakopeshaji walikuwa tayari kufuta/kusamehe deni hilo.

# 5.Kutolipa madeni unayodaiwa ni ghali


Katika miaka ya 1980 Tanzania ilikopa dola za marekani milioni 49 kutoka Brazili ili kugharimia mradi wa ujenzi wa barabara inayounganisha Morogoro na Dodoma. Deni hilo halikulipwa. Ilipofika mwaka 2010, deni lilikuwa limeongezeka hadi kufikia dola za Marekani milioni 240. Bahati njema kwa Tanzania ni kwamba baada ya mazungumzo ya muda mrefu, hivi karibuni viongozi wa Brazili walikubali kulifuta deni hilo.[3]

Iwapo serikali ya Tanzania itakopa Shilingi za Tanzania bilioni 2,128.8 kwa masharti ya kibiashara katika mwaka 2010/11 na fedha hizo zisilipwe kwa wadai kama makubaliano yanavyosema, inawezekena kwamba baada ya muongo mmoja fedha hizo zitafikia kiasi ambacho itakuwa vigumu sana kwa Tanzania kuzilipa. Mathalan, iwapo mkopo utatozwa riba ya asilimia 5 kwa mwaka, zinazopaswa kulipwa kila mwezi na mkopo huo usilipwe, katika kipindi cha miaka 10 kiasi hicho kitakuwa kimeongezeka kwa asilimia 65% na deni litaongezeka maradufu katika kipindi cha miaka 15.

Kutolipa deni unalodaiwa ni ghali. Jinsi muda mrefu unavyopita bila kutimiza wajibu wa malipo ndivyo riba inavyozidi kukua. Deni ambalo Serikali ya Tanzania ilikuwa inadaiwa na Brazili ni mfano dhahiri unaoonesha jinsi hali inavyoweza kuwa mbaya. Hatari hii inajitokeza zaidi katika mikopo ya kigeni inayotolewa kwa masharti ya kibiashara ambayo kwa kawaida haina muda wa unafuu (grace period) wa kufanya malipo na hutoza viwango vikubwa vya riba.

Wasiwasi mwingine ni iwapo Tanzania itamudu kutimiza wajibu wa kulipa madeni yake kwa wakati. Kwa sasa inashindwa kulipia madeni yake yote, na kuendelea kukopa kibiashara kunaweza kuiingiza nchi katika hali ngumu zaidi. Ilipofika mwezi Juni 2010, nchi ilikuwa imelimbikiza malipo ya nyuma ya kiasi cha dola za Marekani milioni 2,760.8 (au shilingi trilioni 3.8). Sehemu kubwa ya malipo hayo ilikuwa ni riba ambayo haikuwa imelipwa (Tazama Kielelezo cha 3).

**Kielelezo cha 3: Malipo ya kuhudumia deni la Tanzania ambayo yamelimbikizwa, 1998-2010**




**Chanzo:** Majarida ya takwimu ya Benki Kuu ya Tanzania

Inawezekana kuuza dhamana mpya ili kulipia dhamana na hatifungati zilizoiva kwa upande wa madeni ya ndani kwa sababu ulipaji unafanywa kwa kutumia sarafu ileile. Lakini suluhisho hilo si la kutegemewa wakati nchi inapolipa madeni ya nje. Hii ni kwa sababu ni lazima madeni hayo yalipwe kwa kutumia fedha za kigeni na hivyo nchi huwa hatarini kujikuta ina limbikizo kubwa la deni pale

viwango vya kubadili fedha vinapobadilika na thamani ya sarafu yake kushuka. Madeni mapya ya kibiashara ni lazima yalipwe kwa wakati uliopangwa.

## 6. Tanzania inaweza kuwa na uwazi zaidi

Huenda likatokea jambo zuri kwa Tanzania kutokana na ukopaji wa kibiashara, nalo ni juu ya kuongezeka kwa viwango vya uwazi kuhusu mali za nchi, dhima, vilevile bajeti ya nchi. Inawezekana wakopeshaji wa kibiashara wakadai umakini zaidi kwa upande wa Serikali ya Tanzania katika kuzingatia uwazi na kuweka bayana majukumu yake kifedha kuliko wafadhili wa kimataifa ambao maamuzi yao hutegemea mitazamo/maslahi ya kisiasa waliyo nayo.

Kwa kufanya kazi na wakopeshaji wa kibiashara, Serikali inaweza kulazimika kutoa taarifa za kuaminika na pengine kutoa taarifa na takwimu kamilifu zaidi kuhusu bajeti yake, mchanganuo wa bajeti, majukumu, mali na dhima, dhamana na kadhalika kwa uwazi zaidi kuliko ilivyo sasa.[4]

## 7. Hitimisho

Bila shaka inawezekana kuchukua mikopo mipya kibiashara. Lakini ukopaji huo ni jambo ambalo halipaswi kufanywa bila kufikiri kwa makini. Haifahamiki iwapo katika siku zijazo wakopeshaji watakuwa tayari tena kutoa misamaha ya madeni kwa nchi zinazoshindwa kumudu madeni yake. Zaidi ya hayo sifa ya Kitaifa itaifanya Tanzania isitake kuomba tena msamaha kutoka kwa wakopeshaji wake. Maana yake ni kwamba wakati Tanzania inapotaka kuingia katika mikataba mipya ni lazima ihakikishe kuwa inafanya uangalifu mkubwa zaidi katika kupatana masharti, kutumia kwa makini mikopo hiyo katika kuwanufaisha wananchi wake, na kujitahidi kudumisha viashiria vya ulipaji madeni katika hali endelevu.

---

[1] Dambisa Moyo (2009). *Dead Aid: Why aid is not working and how there is a better way for Africa*, London, Allen Lane

[2] *Tathmini ya pamoja ya Mfuko wa Fedha wa Kimataifa ( IMF) na Benki ya Dunia inategemea uwezo wa Tanzania kutekeleza mkakati unaofaa wa usimamizi wa deni la taifa, umakini katika kuchukua mikopo inayotolewa kwa masharti ya kibiashara, na kufanyika kwa tathmini yakinifu zilizo makini zaidi katika miradi/uwekezaji itakayofanya.* Tafsiri yetu kutoka IMF (2010), IMF Country report No. 10/173.

[3] http://www.thecitizen.co.tz/component/content/article/37-tanzania-top-news-story/2836-brazil-leader-offers-240m-debt-waiver.html

[4] Kwa mfano, tathmini ya Uwazi wa michakato ya bajeti kimataifa [(the Open Budget Index (OBI)] inaonesha kwamba Tanzania ina kiwango kisichokidhi cha uwazi katika mchakato wake wa uandaaji na utekelezaji wa bajeti. Tazama: http://openbudgetindex.org/files/cs_tanzania.pdf